

Jinsi ya Kufanya Kipimo cha Kujipima Mwenyewe cha Antijeni za COVID-19 cha Intrivo On/Go

HATUA YA 1. Chukua kipimo katika eneo la upimaji.

HATUA YA 2. Kagua maelekezo yote yanayohusiana na kipimo.

HATUA YA 3. Jipime nje ya eneo la huduma na usubiri kwa dakika 10-15 kupata matokeo yako.

HATUA YA 4. Ripoti matokeo katika healthvermont.gov/reportresults na ujaze fomu fupi.

Jibu lako ni siri.



HATUA YA 5. Endapo uthibitisho wa matokeo ya kipimo chako unahitajika, pakua Programu Tumizi ya On/Go. Ni muhimu kuripoti matokeo ya kipimo chako.



Kwa maelekezo ya kufanya vipimo yaliyotafsiriwa na video za mafunzo, tafadhali tembelea

www.healthvermont.gov/covid-19/testing

cic
Health


VERMONT
DEPARTMENT OF HEALTH

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa Mara

Kipimo cha Kujipima Mwenyewe cha Antijeni za COVID-19 cha Intrivo On/Go ni nini? Kipimo cha Kujipima Mwenyewe cha Antijeni za COVID-19 cha Intrivo On/Go ni kipimo cha biokemia cha haraka kinachokusudiwa kutambua antijeni ya protini ya nukleokapsidi kutokana na SARS-CoV-2 kutoka kwa watu walio na au wasio na dalili au sababu zingine za magonjwa ya mlipuko ili kushuku maambukizi ya COVID-19 wanapopimwa mara mbili katika siku tatu na angalau saa 36 baina ya vipimo. Kipimo hiki kimeidhinishwa kwa matumizi ya nyumbani yasiyo na maelekezo ya daktari kwa kutumia sampuli unazokusanya mwenyewe moja kwa moja kutoka kwenye usufi wa pua (matundu ya pua) kwa watu walio na umri wa miaka 14 au zaidi, au sampuli za usufi wa pua zinazokusanywa na mtu mzima kutoka kwa watoto walio na umri wa miaka miwili au zaidi.

Je, Kipimo cha Kujipima Mwenyewe cha Antijeni za COVID-19 kinalinganishwa vipi na kipimo cha maabara kinachotambua maambukizi kwa kupima RNA zenye virusi? Vipimo vya antijeni ni mahususi sana kwa virusi, lakini havina usahihi wa juu kama ilivyo kwa vipimo vya maabara vya utambuzi maambukizi kwa kupima RNA zenye virusi. Hii ina maana kwamba matokeo chanya huwa ni sahihi, lakini matokeo hasi hayamaanishi hakuna maambukizi.

Je, kipimo changu kinaisha muda wa kutumika lini? Kwa sasa, uhai wa kipimo kutumika unaiisha katika tarehe ya mwisho ya mwezi uliochapishwa kwenye sanduku lako (yaani Januari 2022 inamaanisha tarehe 31 Januari, 2022). Hata hivyo, kwa bidhaa za tiba chini ya EUA, kama vile On/Go, FDA, baada ya kufanya uchunguzi kwa ukaribu, hutoa ongezeko la muda wa kutumika kwa vipimo. Tembelea wavuti hii kwa maelezo ya kina na tazama orodha kamili ya nyongeza ya muda www.letsongo.com/product-updates

Kwa nini kuna vipimo viwili kwenye kifurushi? Kwa mujibu wa On/Go, kipimo kimeundwa kwa matumizi ya bila maelekezo ya daktari/kutumia mwenyewe wakati watu wanajipima mara mbili ndani ya siku tatu, na angalau saa 24 (na si zaidi ya saa 48) baina ya vipimo hivi viwili. Vipimo viwili vilivyojumuishwa huwawezesha watu binafsi kutimiza matumizi yaliyopendekezwa.

Je, ninapaswa kufanya nini ikiwa matokeo ya kipimo changu ni chanya? Iwapo utathibitishwa kuwa una virusi, hakikisha kuwa umeripoti matokeo yako kupitia kiungo-mtandao kilichopo upande mwingine wa kadi hii. Kwa mwongozo wa ziada, tembelea healthvermont.gov/covid19positive



Kupata maelezo zaidi juu ya Kipimo cha Kujifanyia Mwenyewe cha Antijeni za COVID-19 cha Intrivo On/GO, tembelea www.letsongo.com/faq

3/1/2022